

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

614

MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 3

Mwaka: 2022

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **kumi na nne (14)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Sehemu A in alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Soma **maelekezo yote** yaliyopo kwenye kijitabu cha kujibia.
5. Vifaa vya maswaliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Katika wasilisho lake, mkufunzi wa somo la Jiografia alisema kuwa, mwinuko kutoka usawa wa bahari, mikondo ya bahari, latitudo na umbali wa eneo kutoka baharini hufanya maeneo kuwa na tabia nchi zinazotofautiana. Eleza kwa kifupi ni kwa namna gani mambo hayo yanasababisha tofauti hizo.
2. Matukio mbalimbali ya kiasili yanaweza kumsababishia binadamu majanga kwa namna mbalimbali. Kwa kutumia hoja nne, oneshwa kwa kifupi namna matukio hayo yanavyoweza kusababisha majanga.
3. Katika kuelewa mambo ya kijiografia, mistari ya longitudo na latitudo hutumika. Baadhi ya mistari hiyo ni pamoja na mstari wa Ikweta, mstari wa kansa, mtari wa kaprikoni na mstari wa Greenwich. Eleza kwa kifupi umuhimu wa kuelewa dhana ya kila mstari katika maisha ya binadamu.
4. Katika moja ya semina kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia, wanasemina walihitimisha kuwa, upimaji na tathimini ni kitu muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo. Kwa kifupi, unga mkono hitimisho hilo kwa kutoa hoja nne.
5. Kutokana na kugundulika kwa madini ya dhahabu karibu na mji mmoja, kulijitokeza changamoto nyingi za makazi katika mji huo. Kwa kutumia hoja nne, bainisha mbinu nne zinazoweza kutumika katika kukabiliana na changamoto hizo.
6. Wakati wa ujio wa wakoloni katika Bara la Afrika, waafrika chini ya viongozi mbalimbali walipinga uvamizi huo. Hata hivyo, waafrika walishindwa katika harakati zao. Eleza kwa kifupi mafunzo manne ambayo waafrika wanaweza kujifunza kutokana na kushindwa kwao.
7. Wavumbuzi, wamisionari na wafanyabiashara walikuja Afrika ili kuleta ustaarabu mpya na siyo kwa maslahi ya kiuchumi kama inavyodaiwa na wanahistoria. Kwa kifupi, pinga usemi huu kwa kutoa hoja nne.
8. Mwalimu mkuu wa shule amekupanga kufundisha mada ya mifumo ya uzalishaji mali wakati wa zama za chuma. Ni mambo gani manne utakayozingatia wakati wa uandaaji wa zana za kufundishia?
9. Katika baadhi ya mataifa ya kiasia kama vile, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudani Kusini na Somalia bado kuna matukio ya migogoro ya kisiasa ambayo husababisha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe. Eleza kwa kifupi athari nne zinazotokana na migogoro hiyo.

10. Baada ya vifa vya FIM vya Dunia, kuliundwa Umoja wa Mataifa. Kwa kutumia hoja nne eleza kwa kufupi malengo ya kuundwa kwa umoja huo.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

11. Pamoja na kwamba jamii nyingi za Kiafrika zilipinga uvamizi wa kikoloni, wavamizi walifanikiwa na hivyo kuanza hatua mpya ya kuimarisha uchumi wa kikoloni. Kwa kutumia mifano, chambua shughuli tano kuu za kiuchumi zilizofanywa katika hatua hiyo.
12. Uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia somo la Historia bado ni tatizo linalojitokeza katika baadhi ya shule za msingi na hivyo kusababisha ugumu katika ufundishaji na ujifunzaji. Eleza njia tano anazoweza kutumia mwalimu katika kutatua changamoto hiyo.
13. Katika majadiliano ya wanafunzi kuhusu umbile la dunia wapo waliosema kuwa "Dunia ni duara" na wengine walikuwa na mashaka hivyo kutaka uthibitisho. Kwa kutumia hoja tano, thibitisha kuwa dunia ni duara.
14. Njia ya majadiliano ya vikundi ni kati ya njia shirikishi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Jiografia. Eleza kwa ufasaha mambo matano ya kuzingatiwa na mwalimu wakati wa matumizi ya njia hiyo darasani.